SERA YA UTAWALA
Kuziia kujiua na Kuingilia Kati
INS-A038

Policies are periodically revised. For the most recent version, please visit https://salkeiz.sharepoint.com/qam/SitePages/Home.aspx

1. Wilaya ya Salem-Keizer inajidhatiti kwa afya na usalama kwa wanajumiya yote ya shule. Hizi sera zinalinda matukio yaliyofanyika shule, kwenye maeneo ya shule,na kwenye shughuli za michezo inayodhaminiwa na shule, kwenye basi au gari na kwenye vituo vya basi na matukio yanayodhaminiwa nje ya shule na wakati wafanyakazi wa shule wanakuwepo. Hii sera inatumika kwa jamii yote ya shule, kujumuisha waelimishaji, shule na wafanyakazi wa wilaya, wanafunzi na wazazi/walezi. Wale wanajitolea wataelekezwa na shule au mfanyakazi wa wilaya kwa vile hii sera inawahusu. Sera hii pia itashughulikia majibu yanayofaa kwa shule kujiua au tabia za hatari kubwa ambayo hufanyika nje ya mazingara ya shule pale inapoarifiwa.

2. Kuzuia

2.1. Utekelezaji wa sera katika wilaya – Mshauri wa ngazi ya wilaya kwenye mambo ya kujiua na aliyetuliwa na msimamizi mkuu wa mashule au anayetakiwa. Huyu anaweza kuwa ni tayari mfanyakazi.

2.2. Mshauri wa wilaya kwenye kuzuia kujiua atakuwa na jukumu la kupanga na kuratibu utekelezaji wa hii sera kwa shule za wilaya.

2.3. Kila msimamizi wa shule atachagua mfanyakazi katika shule kusimamia matatizo yanayohusiana na kuzuia kujiua na sera za utekelezaji. Huyu anaweza kuwa ni tayari mfanyakazi.

2.4. Wafanyakazi wote watatakiwa kutoa taarifa ya wanafunzi wanaoamini kuwa wako katika hatari ya kujiua kwa msimamizi wa shule na au/mtu aliyeteuliwa katika wanafanyakazi.

2.5. Wafanyakazi wa shule watafanya ndani ya mamlaka waliyonao kulingana na hati au leseni walizonazo. Hii sera hairuhusu au kuhamasisha mfanyakazi wa shule kugundua au kuponya magonjwa ya akili isipokuwa pale tu kama mfanyakazi ana leseni na ameajiriwa kufanya hivyo.

2.5.1. Kwenye shule jaribio la kutaka kujiua mfanyakazi anatakiwa kufuata hatua kwenye INSW054 – Jaribio la kujiua shuleni na jaribio la kujiua nje ya shule mfanyakazi lazima kufuata INS-W055

2.6. Maendeleo ya taaluma kwa wafanyakazi –Wafanyakazi wote watapokea mafunzo ya mwanzo ya masaa mawili uso kwa uso katika kujifunza kuzuia kujiua.

2.7. Baada ya mafunzo ya awali, maendeleo ya kitaaluma kila mwaka kwenye vigezo vya hatari, dalili za kuangalia, sababu ya kinga, utaratibu wa kujibu, marejeo, kuzuia na rasilimali kuhusiana na kuzuia kujiua kwa vijana vitatolewa. Taaluma ya maendeleo itajumuisha makundi ya wanafunzi wanaonyesha hatari ya kujiua pamoja na wale wanaishi na matatizo ya magonjwa ya akili au shida za utumiaji madawa, wale wanaojihusisha na kujiumiza au kujaribu kujiua, wale wanaondoka nyumbani mara kwa mara, wale wanaopata shida ya kutokuwa na makazi, wanafunzi wa American Indian/Alaska Native, LGBTQ wanafunzi (msagaji, shoga, jinsia mbili, jinsia na wale ambao hawajaamua) wanafunzi waliofiwa na ndugu zao kwa kujiua na wale matatizo ya ugonjwa au aina fulani ya ulemavu.

2.7.1. Mafunzo ya taaluma ya ziada yatatolewa kwenye kutathmini hatari na mgogoro wa kuingilia kati, kwa mtu aliyechaguliwa wa shule katika kusimamia kuzuia kujiua.

2.8. Programu kwa vijana kuzuia kujiua – Maendeleo na mwongozo wa vifaa vya elimu inayolenga mwanafunzi kuanzia K-12 itajumuishwa kwenye mtaala. Mtaala huu na vifaa utazingatia kulingana na umri 1) Uchaguzi na mkakati wa kukabiliana ni muhimu kwa usalama na afya. 2) Jinsi ya kutambua sababu za hatari na ishara kwenye shida ya afya ya

akili na kujidhuru binafsi au watu wengine 3) kusaidia kuweka mikakati kwa mtu au watu na kujumuisha jinsi ya kufanya kushirikikisha rasilimali za shule na kuomba msaada kwa rafiki. Na kuongeza, shule inaweza kuweka makundi madogo madogo ya ziada katika kuzuia kujiua katika programu ya wanafunzi.

2.9. Uchapishaji na Usambazaji – Hii sera itakuwa inachapishwa kila mwaka na kuhusisha wanafunzi wote na walimu kwenye kitabu cha shule na kwenye tuvuti ya wilaya.

3. Tathamini na Rufaa

3.1. Pale ambapo mwanafunzi atatambuliwa na mfanyakazi kama anauwezo wa kujiua kama vile kuongelea wazi, kuonyesha wazi sababu kama uchochezi au ulevi, vitendo vya kujiumiza vinatokea au mwanafunzi amejirufaa mwenyewe, mwanafunzi ataonwa na msimamizi au mtu aliyechaguliwa kufanya ngazi ya 1 tathmini ya hatari ya kujiua (SRA)

3.2. Kwa vijana walio katika hatari ya kujiua au kujidhuru:

3.2.1. Wafanyakazi wataendelea kumuangalia mwanafunzi kwa kuhakikisha usalama wake.

3.2.2. Mkuu wa shule na mratibu wa kuzuia kujiua watajulishwa na tukio mara tu itakapowezekana.

3.2.3. Mfanyakazi aliyechaguliwa na shule au msimamizi atawasiliana na mzazi au mlezi wa mwanafunzi kama ilivyoelezewa kwenye kipengele cha taarifa na ushiriki wa wazazi.

3.2.4. Fomu ya mahojiano itakamilishwa, na mzazi/mlezi, na familia watasaidiwa kwa kupanga mpango salama kulingana na tathmini ya hatari ya kujiua. Pale itakapokuwa ni sawa, hii inaweza kujumuisha kupiga simu huduma ya dharura, kumpeleka mtoto karibu na huduma za hospitali au kutumia ushirikiano wa kata kwenye afya ya akili kumalizia kufanya tathmini ya hatari ya kujiua (SRA)katika ngazi 2 hapo hapo

3.2.5. Mfanyakazi ataomba mzazi au mlezi wa mwanafunzi kuandika ruhusa ya maandishi kuongelea afya ya mwanafunzi kwa watoa huduma wa nje.

4. Utaratibu wa Kuingia tena baada ya shida ya afya ya akili

4.1. Kwa wanafunzi wanaorudi shuleni baada ya shida ya afya ya akili (mfano., jaribio la kujiua au kulazwa kwa wagonjwa wa akili) msimamizi au mfanyakazi aliyeteuliwa atakutana na mzazi au mlezi wa mwanafunzi na pale panapofaa, kututana na mwanafunzi na kutengeneza mpango salama wa kumsaidia mwanafunzi na wanafanyakazi.

4.1.1. Msimamizi au mfanyakazi aliyeteuliwa ndiyo atakaye kuratibu kurudi kwa mwanafunzi au na mzazi/mlezi wao. Msimamzi au mfanyakazi aliyeteuliwa ataomba kibali cha kuratibu na mtoa huduma ya afya ya akili wa nje.

4.1.2. Shule au wilaya itaomba mzazi/mlezi kutoa nyaraka za kujitolea kutoka kwa mtoa huduma ya afya ya akili kwamba mwanafunzi amepata uchunguzi na sasa siyo hatari kwake na watu wengine

4.1.3. Usiri ni muhimu ili kumlinda mwanafunzi na kumwezesha mtu wa shule kutoa msaada. Msimamizi au mfanyakazi aliyeteuliwa ataongea na mzazi au mlezi wa mwanafunzi taarifa ambazo mfanyakazi wa shule atahitajika kujua kumsaidia mwanafunzi kielimu, kijamii, kihemko na mahitaji ya kimwili.

4.1.4. Mfanyakazi aliyeteuliwa atakuwa anamwangalia mwanafunzi kila baada ya muda pamoja na mzazi au mlezi kuweza kumsaidia mwanafunzi kujiweka sawa katika jamii ya shule na kuzungumzia kama kuna wasiwasi unaoendelea.

4.2. Mwanafunzi aliyefiwa kwa majaribio ya kujiua atasaidiwa na msimamizi wa shule au mshauri wa wafanyakazi.

Taarifa kwa mzazi na Ushirikishwaji

4.3. Katika hali inayotathmini hatari ya kujiua kwa mwanafunzi au amejaribu kujiua, wazazi au walezi wa mwanafuzni watapewa taarifa na msimamizi wa shule, yule aliyetuuliwa au mshauri wa afya ya akili isipokuwa pale sehemu ya 5.4 inatumika.

4.4. Kama mwanafunzi ataonyesha tabia au kitendo cha kujiua, mzazi au mlezi ashauriwe kwenye “inamaanisha kizuizi” kumzia mtoto njia ya kujaribu kujiua.

4.5. Mfanyakazi ataomba ruhusa kuongea na mtoa huduma wa afya ya akili kuhususiana na mtoto wako.

4.6. Kupitia maongezi na mwanafunzi, msimamizi au mtu eliyeteuliwa ataangalia kama kuna uwezekano mbeleni wa kujizuru kutokana na taarifa za mzazi au mlezi. Na kama msimamizi, mtu aliyeteuliwa au mtoa huduma wa afya ya akili anaamini katika uwezo wake wa kitaaluma kuwa kuwasiliana na mzazi au mlezi kuna uwezekano wa kuleta madhara au ustawi wa mwanafunzi, unaweza kuchelewa kuwasiliana na mzazi au mlezi mpaka wakati muafaka. Na kama kutachelewa na sababu ya kuchelewa iandikwe. Na kama ni muhimu, mamlaka husika itataarifiwa.

5. Kuepusha tukio la kifo kwa kujiua

5.1. Kuafuatia kifo cha mwanafunzi kwa kujiua, msimamizi au timu ya matatizo inatengeneza hatua za mpango kuwaongoza shule kujibu kutokana na mwongozo wa timu ya matatizo. Hatua za mpango zinajumuisha, lakini siyo haya tu:

5.1.1. Msimamizi atawasiliana na familia ya wafiwa kutoa msaada.

5.1.2. Msimamizi atawasiliana na ofisi ya jamii na mahusiano kwenye masiliano kuwataarifu ofisi mbalimbali na kuangalia timu ya matatizo inakavyojibu.

5.1.3. Msimamizi, ofisi ya jamii na mahusiano na mawasiliano na timu ya matatizo watatathmini tatizo kuangalia jinsi ya msaada.

5.1.4. Mfanyakazi aliyeteuliwa atashirikiana na wakala wa mitaa kwenye afya ya akili (LMHA) na wasimamizi kuanzisha huduma ya msaada kwa jamii ya shule iliyoathirika.

6. Mapitio ya Vitendo vya Kuingilia Kujiua

6.1. Mtu anaweza kuomba wilaya ya shule kupitia hatua za shule kujibu kuhusiana na hatari za kujiua kwa kuwasiliana na muhusika katika ngazi ya ukurugenzi

6.2. Mapitio yote yatayatafakari hali ya mwanafunzi na haki za shirikisho chini HIPAA na FERPA na sheria ya usiri kwa mfanyakazi.

Implementing Procedures:

Revision History:

Date	Description

Approved By:_____